# Usalama wetu ?

## Maoni ya wananchi juu ya usalama na haki








## 1. Utangulizi

Mwezi Desemba mwaka 2014, Tanzania ilifanya uchaguzi wake wa serikali za mitaa. Hata hivyo, "dosari na makosa mbalimbali'', viliwatia hofu wapiga kura na wanaharakati wa demokrasia: vifaa vya uchaguzi havikusambazwa kama inavyotakiwa, na umati wa watu walijikusanya karibu vituo vya kupigia kura katika jitihada za kuhakikisha kura zao zinahesabiwa (The Citizen, 15 Mei 2014). Mwezi Januari 2015, kundi la vijana wahalifu lililojulikana kama "Panya Road", liliibuka jijini Dar es Salaam na kuleta wasiwasi mkubwa kwa kufanya matukio ya uporaji, wizi na vurugu. Kuibuka kwa kundi hili kuliibua taarifa na maoni mengi katika vyombo vya habari - hasa mitandao ya kijamii na hatimaye, mamia ya vijana hao walitiwa nguvuni na jeshi la polisi. (The Citizen, Januari 6, 2015).

Kutokana na matukio haya, je wananchi wanajihisi kuwa salama majumbani mwao?
Je, wanaweza kuhisi wako salama ifikapo wakati wa kupiga kura? Tishio la kikundi cha Panya Road kwa namna nyingine, linaweza kuwa limekuzwa kuliko hali halisi. Hata hivyo, mtazamo wa usalama – kuhisi uko salama - ni muhimu sana kama ilivyo muhimu kujua uwezekano halisi wa kuvamiwa au kuibiwa. Kama watu wanahisi hawako salama ndani ya jamii zao, wataacha kufanya shughuli zao: wataepuka baadhi ya maeneo au muda fulani wa siku husika. Hii inaweza kusababisha kupungua kwa shughuli za kiuchumi.

Muhtasari huu unaripoti takwimu zenye uwakilishi wa kitaifa kutoka Tanzania bara kuhusu maoni ya wananchi juu ya usalama na haki kwenye jamii zao. Takiwmu zimetokana na awamu ya 30 ya *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika mara kwa mara kwa njia ya simu za mkononi (www.twaweza.org/sauti). Jumla ya wahojiwa 1,401 walifikiwa kati ya Februari 13 na Machi 3, mwaka 2015. Ili kufuatilia mwenendo baada ya muda, takwimu kutoka utafiti wa awamu ya nane (zilizokusanywa kati ya Oktoba 03-17 mwaka 2013; wahojiwa 1,662 ) zimerejewa hapa.

Muhtasari huu umeandikwa na Youdi Schipper, Angela Ambroz, na Elvis Mushi
Na umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Aprili 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Matokeo muhimu ni:


- Mtu mmoja kati ya watatu amewahi kuibiwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.
- Wananchi watatu kati ya kumi wamewahi kusikia kwamba watu wamepigwa mawe au kutishiwa na vikundi vya usalama katika kipindi cha mwaka uliopita
- Matukio ya uhalifu yanayofanywa na vikundi vya watu yamepungua kwa kiasi kikubwa kati ya 2013 na 2015 ila matukio ya ukatili yanayofanywa kwa polisi yameongezeka.
- Wananchi wanne kati ya kumi wangeweza kwenda polisi wanapokumbwa na uhalifu
- Watu wengi (84%) wanaamini kuwa wataathiriwa na makundi ya vijana kama lile la Panya Road - siku zijazo.
- Taasisi inayotembelewa zaidi pale watu wanapokumbwa na uhalifu ni polisi (37%) au asasi ya kiusalama iliyoko maeneo yao (32%) - ingawa pia watu waliamini kuwa polisi na mfumo wa sheria huwahudumia vizuri zaidi watu wenye pesa kuliko masikini
- Takriban watu wawili kati ya kumi (18%) walishuhudia vurugu au vitisho kwenye kituo cha kupigia kura wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi Desemba mwaka 2014.

# 2. Mambo saba kuhusu ulinzi na usalama nchini Tanzania

## Jambo la 1: Wananchi nane kati ya kumi wanahisi wako salama mitaani na majumbani kwao

Kati ya mwaka 2013 na 2015, wananchi wa Tanzania kimsingi wamebaki na mitizamo ileile kuhusu ulinzi na usalama kwenye vitongoji/mitaa yao. Karibu wananchi nane kati ya kumi wanaripoti kutowahi au mara chache sana, kuhisi wako salama ndani ya kipindi cha mwaka jana. Ni 15% tu wameripoti kuwahi kujihisi hawako salama muda mwingi ndani ya mwaka uliopita (Kielelezo cha 1).

**Kielelezo cha 1: Katika kipindi cha mwaka jana, ni mara ngapi ulihisi hauko salama unapotembea mtaani kwako?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015), Awamu 8 (Oktoba 2013)

## Jambo la 2: Wananchi watano kati ya kumi wameshawahi kuibiwa, watatu kati ya hao walikumbwa ndani ya kipindi cha mwaka jana

Zaidi kidogo ya nusu ya wananchi wameshawahi kuibiwa, wengi wao (watatu kati ya kumi, 30%) wakiibiwa nao katika kipindi cha mwaka uliopita (Kielelezo cha 2). Takwimu hizi ni karibu sawa na takwimu zilizokusanywa mwaka 2013. Kwa ujumla, idadi hii ni kubwa kuliko wastani wa Afrika wa watu wanaokumbwa na wizi nyumbani. Vilevile, 'kitisho kwa jamii' kilichotajwa sana ni wizi, wananchi 42% waliripoti hivyo (takwimu hazijaoneshwa).`

**Kielelezo cha 2: Lini mara yako ya mwisho kuibiwa kitu chochote?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015), Awamu 8 (Oktoba 2013)

## Jambo la 3: Wananchi wanaamini makundi ya vijana wahalifu ni tishio kubwa

Mwezi Januari 2015, liliibuka kundi la vijana wahalifu huko Dar es Salaam lililojiita "Panya Road". Kundi hili lilitawala vichwa vya habari magazetini kutokana na kufanya matukio ya uhalifu na kuleta vurugu ndani ya jamii, na kufuatiwa na msako mkali wa jeshi la polisi uliopelekea kukamatwa kwa mamia ya washiriki wa kundi hilo. Habari za uhalifu wa kundi hili zilizagaa nchini na eneo lote la Afrika mashariki. Hivyo, tuliwauliza watu kama walikuwa wamesikia habari za kundi hili: wananchi sita kati ya kumi (60%) walisema wamesikia (takwimu hazijaoneshwa). Aidha, tuliwauliza kama ndani ya jamii zao kuna makundi yoyote yanayofanana na 'Panya road': wengi walisema hapana (87%; takwimu hazijaoneshwa).

Hata hivyo, pale tulipowauliza kama wanaamini mtu binafsi anaweza kuathiriwa na kundi la vijana wahalifu kama 'Panya Road', watu wengi walisema ndiyo - 66% wanaamini "kuna uwezekano mkubwa sana" na 18% wanaamini "kuna uwezekano kwa kiasi fulani" (Kielelezo cha 3).

**Kielelezo cha 3: Unadhani kuna uwezekano gani wa wewe kuathiriwa na kikundi kama Panya road?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015)

## Jambo la 4: Vikundi vya ulinzi vya kijamii vinauwezekano mkubwa wa kusababisha vurugu

Ulinzi na usalama wa jamii siyo tu kazi ya kushughulikia matukio ya uhalifu, lakini pia ni jukumu la msingi la jeshi la polisi. Nchini Tanzania jeshi la polisi lina upungufu wa rasilimali watu na rasilimali fedha. Hii imesababisha jamii kuanzisha mifumo yao wenyewe ya polisi kupitia vikundi vya ulinzi na usalama. Vikundi hivi hutoa walinzi mbadala kuchukua majukumu ya kiusalama kama ya polisi na kuhakikisha sheria zinafuatwa na wananchi. Kwa upande mwingine, makundi haya hayana mafunzo rasmi, na hivyo yanaweza kutuhumiwa kutumia nguvu na kufanya ukatili mwingi, kukiuka haki za binadamu au misingi ya utawala bora.

Wananchi wanaripoti kuwa vikundi hivi vimekuwa mstari wa mbele kutoa vitisho, kupiga watu au kupiga mawe watu mara kwa mara (vikizidi polisi kwa asilimia 8 mwaka 2015). Kiwango cha uhalifu kilichofanywa na wananchi kimebaki kama ilivyokuwa mwaka 2013, lakini uhalifu wa makundi umeshuka kutoka 28% mwaka 2013 hadi 12% mwaka 2015 (Kielelezo cha 4). Katika kipindi hichohicho ukatili wa polisi umeongezeka kutoka 14% hadi 21% (Kielelezo cha 4). Ni muhimu kutambua kuwa haya ni matukio ambayo wananchi wamesikia siyo waliyoshuhudia moja kwa moja au yaliyowafika wao.

**Kielelezo cha 4: Matukio ya vitisho, kupigwa na kurushiwa mawe kulikofanywa na makundi mbalimbali mwaka jana**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015), Awamu ya 8 (Oktoba 2013)


## Jambo la 5: Wananchi wanaamini mfumo wa utoaji haki una upendeleo

Ni mwananchi mmoja tu kati ya watano anayefikiri kuwa watu maarufu au watu wenye hadhi fulani (kama vile watumishi wa umma, viongozi wa dini, maafisa wa polisi na matajiri) wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria ikiwa watafanya uhalifu (Kielelezo cha 5). Takwimu hizi zimeshuka kidogo ukilinganisha na za mwaka 2013: kwa mfano, mwaka 2013 wananchi

39% waliamini kuwa watumishi wa umma wanaweza kukumbana na mkono wa sheria wanapovunja sheria idadi hii imeshuka hadi kufikia 21% mwaka 2015 (Kielelezo cha 5). Wananchi wanaona pengo la utoaji haki linaongezeka kati ya wananchi wa kawaida na watu wenye hadhi fulani katika jamii.

Wananchi wa kawaida wanaamini kuwa wao wana uwezekano mkubwa zaidi wa kukumbana na mkono wa sheria kuliko watu wenye hadhi fulani kwenye jamii: nusu yao wanafikiri kuwa wananchi wa kawaida wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria pindi wanapofanya uhalifu au kosa la jinai. Takwimu hizi kwa kiasi kikubwa hazijabadilika tangu mwaka 2013. Hakika, kwa kila kundi la watu katika jamii, wananchi wanaamini kuna uwezekano mdogo kwa wahalifu kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Hii inaonesha wananchi wana imani ndogo na ufanisi wa mfumo wa sheria hapa nchini.

**Kielelezo cha 5: Je, unadhani kuna uwezekano gani wa makundi yafuatayo kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria wakifanya kosa?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015)


Walipoulizwa ni kundi gani (kutoka kwenye orodha waliyopewa) linahudumiwa vyema na jeshi la polisi, wananchi sita kati ya kumi (60%) walitaja kundi la matajiri, na mmoja kati ya kumi (10%) walitaja wanasiasa (takwimu hazijaoneshwa).

## Jambo la 6: Wananchi wengi wana imani ndogo na jeshi la polisi

Mwananchi akikumbwa na uhalifu, atamkimbilia nani? Licha ya kufikiri kuwa mfumo wa haki haufanyi kazi vizuri na kuona ongezeko la matukio ya ukatili wa polisi, wananchi wanne kati ya kumi (37%) walisema wangekwenda polisi kwanza kupata msaada. Idadi hii inaweza kulinganishwa na wananchi tatu kati ya kumi (32%) waliosema watakwenda kwanza kwenye kamati za ulinzi za mitaa au vikundi vya ulinzi na usalama vya kijamii. Mahali pengine ambako kwa kiasi kidogo wananchi wangekwenda kupata msaada ni kwa mwenyekiti wa kijiji, familia au marafiki.

Tulipowauliza wananchi mitazamo yao ya kwanini watu hawaripoti taarifa za uhalifu kwa jeshi la polisi? Wananchi 29% walidai ni kutokana na rushwa (Kielelezo cha 6). Hii inashabihiana na matokeo ya huko nyuma ya utafiti wa *Sauti za Wananchi* ambapo polisi ilitajwa kama taasisi kinara zaidi kwa rushwa hapa nchini [1]. Sababu ya pili iliyotajwa na wahojiwa ni kwamba polisi hawasikilizi au hawajali taarifa/malalamiko ya wananchi (Kielelezo cha 6).

**Kielelezo cha 6: Je, unafikiri ni sababu gani inayowafanya watu wasitoe taarifa za uhalifu polisi?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015)


## Jambo la 7: Wananchi wawili kati ya kumi walishuhudia vurugu kwenye kituo chao cha kupigia kura wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa

Tuliuliza njia mbalimbali ambazo vurugu za kisiasa zinaweza kujionesha: wakati wa maandalizi ya uchaguzi (kupitia, kwa mfano, vitisho au kutia hofu), na wakati wa uchaguzi wenyewe, iwe katika vituo vya kupigia kura au kwenye jamii kwa ujumla .

Wananchi wawili kati ya kumi wanaripoti kuwa walishuhudia vurugu au vitisho kwenye vituo vyao vya kupigia kura wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi Desemba 2014 (Kielelezo cha 7). Idadi kama hiyo walishuhudia vurugu katika jamii zao, na mwananchi moja kati ya kumi aliripoti kushuhudi vurugu katika jamii zao kipindi cha kuelekea kwenye uchaguzi (Kielelezo cha 7).

[1] *Sauti za Wananchi*, Muhtasari Na. 14. Je, kuongezeka kwa sheria, mashirika na ahadi nyingi dhidi ya rushwa vinaleta mabadiliko? Mitazamo ya watu juu ya rushwa nchini Tanzania; Agosti 2014.

**Kielelezo cha 7: Kushuhudia vurugu au vitisho vinavyohusiana na uchaguzi**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 30 (Februari-Machi 2015)

Nusu ya wananchi walidai kuwa vyama vya siasa kwa ujumla wake vilikuwa na dosari kadhaa lakini hawakutaja majina ya vyama hivyo. Wananchi wawili kati ya kumi (18%) walikaa kwenye vituo vya kupigia kura wakati na baada ya zoezi la kupiga kura, hasa kwa sababu walitaka wawepo wakati wa kutangaza matokeo (61% ya waliokaa vituo vya kupigia walitoa sababu hii). Lakini wahojiwa wachache (24% ya waliokuwa vituo vya kupigia kura na 4% ya jumla ya watu) walitoa sababu ya kukaa vituoni kuwa ni kutaka kulinda kura zao.

Isitoshe wananchi mmoja kati ya nne (27%) walisema wana mpango wa kukaa kwenye vituo vya kupigia kura wakati wa kura ya maoni ya katiba mpya (takwimu hizi zilikusanywa kabla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza kuahirishwa kwa kura ya maoni). Tulipouliza zaidi, wananchi wana maoni gani kuhusu juhudi za NEC kuhakikisha kuna uchaguzi huru na wa haki, wananchi saba kati ya kumi (70%) walikubali kuwa Tume ya Uchaguzi imefanya kazi nzuri kufanikisha hili (takwimu hazijaoneshwa).

## 3. Hitimisho

Kwa ujumla, ripoti zinaonesha kuwa wananchi wanajisikia wako salama zaidi mwaka huu (2015) kuliko walivyokuwa miaka miwili iliyopita (2013). Hata hivyo, bado kuna hisia miongoni mwa watu kuwa mfumo wa sheria huwahudumia vizuri zaidi watu wenye pesa na wale wenye hadhi fulani katika jamii kuliko wananchi wa kawaida. Mara nyingi "mtu wa kawaida" badala yake hutegemea zadi mifumo ya kienyeji zaidi, isiyo rasmi, au mifumo iliyo nusu-rasmi kupata haki zake: Hakika, watu wengi wamewahi kusikia kuhusu mtu kupigwa na vikundi vya ulinzi jamii kuliko polisi, na watu wengi wamevitaja vikundi vya usalama kuwa kimbilio lao la kwanza wanapokumbana na uhalifu. Sababu inayowafanya wananchi wengi kutokwenda polisi kwanza baada ya uhalifu kutokea ni kuwa wanatarajia wataombwa rushwa na polisi. (hoja hii inafanana na matokeo ya utafiti wa Afrobarometer uliofanyika Tanzania mwaka 2012, ambao ilibaini sababu kuu mbili za wananchi kutoripoti uhalifu polisi ni kuombwa rushwa na "polisi kutowasikiliza au kuwapuuza".)

Wakati Tanzania ina sifa ya kuwa nchi ya amani, takwimu kutoka nchi nyingine za Afrika zinaonesha kuwa Watanzania wanaripoti viwango vya juu vya uhalifu (kwa mfano, 36% ya Watanzania wamewahi kukumbwa na wizi nyumbani, ikilinganishwa na 26% ya wastani wa wizi majumbani barani Afrika). Kuna sababu nyingi kwa nini usalama unapaswa kutiliwa kipaumbele kwenye orodha ya vipaumbele vya serikali. Mbali na faida iliyowazi ya kujenga

amani kwenye jamii, usalama wa nchi pia una athari kiuchumi: kama watu wanahisi hawako salama kwenye baadhi ya vitongoji/mitaa, au nyakati fulani ndani ya siku, itasababisha shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo na katika nyakati hizo kupungua au kutofanyika kabisa. Aidha, kila shilingi iliyowekezwa kununulia kufuli na kuwalipa askari (walinzi) haiwezi kutumiwa tena kwa tija kuwekeza kwenye mifugo, mbegu, masoko ya biashara au kompyuta. Hii inasababisha kushuka kwa Pato la Taifa, na kudumaza maendeleo ya chini.

Usalama wa mtu ni suala jingine muhimu. Kwa mara ya kwanza katika historia, Tanzania imepanga kufanya mambo mawili, kura ya maoni ya kitaifa na uchaguzi mkuu mwaka huu huu wa 2015. Matukio haya ni muhimu sana kwa wananchi wa kawaida kuamua juu ya hatma ya taifa lao na uchaguzi wa viongozi wao kwa miaka mitano ijayo. Lakini wakati huo huo ni muhimu sana kwa wao kujisikia wako salama wakati wa kutumia haki yao ya kidemokrasia-kupiga kura. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, wananchi wawili kati ya kumi (18%) walishuhudia vurugu kwenye kituo cha kupigia kura. Miongoni mwa walioshuhudia vurugu hizo, mmoja kati ya wawili aliamini chama fulani cha siasa kilikuwa na makosa. Pamoja na idadi ndogo, ni muhimu tukajiuliza kama tishio hili la vurugu linazuia haki za watu kupiga kura katika nchi ambapo zaidi ya nusu (52%) ya watu wanaishi mbali na vituo vya polisi - na hivyo, wanatarajia ulinzi mdogo wa umati mkubwa wa watu siku ya uchaguzi.

Hivyo, nini kifanyike? Bila shaka, serikali itahitaji kutumia mbinu mbili za haraka: kushughulikia vyote, matukio halisi ya uhalifu, vile vile mitazamo kuhusu uhalifu. Kwa sasa, kuna mtazamo hasi: wananchi hawajaona maboresho yoyote kwenye mitizamo yao kuhusu usalama wa jamii tangu mwaka 2013. Licha ya polisi kuwatia nguvuni kundi kubwa la vijana wahalifu wa Panya Road, kwa mfano, idadi kubwa ya wananchi (84%, rejea jambo la 3) wanatarajia kuathiriwa na kundi la vijana wahalifu kama panya road siku zijazo. Kwenye takwimu za utafiti wa nyuma wa *Sauti za Wananchi*, tuliona kuwa jeshi la polisi lilionekana kuwa taasisi yenye rushwa zaidi nchini. Aidha, wananchi wanaamini kosa moja tu la jinai kati ya mawili ndo linaweza kufikishwa kwenye mfumo wa mahakama – uwezekano ni mdogo zaidi kama kosa hilo limefanywa na ‘’kigogo”.

Watu wakimbilie kwa nani watapokuwa na tatizo kama siyo polisi? Kwa wenye pesa, sekta ya ulinzi imeanzisha makampuni binafsi ya ulinzi kutoa huduma za ulinzi na usalama badala ya jeshi la polisi lenye askari wazembe na wala rushwa. Kwa wananchi maskini, kuna vikundi vya kijamii vinavyolinda maeneo yao. Mwananchi mmoja kati ya kumi (12%) bado anaripoti kushuhudia mtu akipigwa na ‘kundi’ la watu (idadi imeshuka kutoka 28% mwaka 2013; rejea jambo la 4). Wananchi 7% wamewahi kuona mtu akiuawa na kundi la walinzi jamii. Hata hivyo, adhabu hizi zinazovuka mamlaka ya mahakama, hazina hukumu, hazina majaji wala baraza la wazee wa mahakama, na ni hivyo hakuna haki rasmi kwa mtu. Hatari ni kubwa maana watu wasio na hatia wanaweza kutuhumiwa tu kuwa ni “wezi” na wakashambuliwa na kuuawa au kuumizwa. Ki-usawa, je, taratibu za kudai haki za kijamii, zilizo nusu rasmi na zisizo rasmi ni bora kuliko taratibu rasmi za kisheria zilizo mbali na wananchi?

Kushughulikia masuala haya - ikiwa ni pamoja na kurejesha imani ya watu kwenye mfumo rasmi wa sheria na haki, kupitia juhudi za pamoja kuboresha mapambano dhidi ya vitendo vya uhalifu na “mahusiano ya umma” kuwa sehemu ya polisi - itakuwa hatua muhimu kwa maendeleo ya Tanzania.